

HEKO KILOSA NA HATI SAFI

Halmashauri ya wilaya ya Kilosa ni miongoni mwa Halmashauri 138 zilizopata hati safi kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 na kuwa mfano bora wa kuigwa kwa mkoa wa Morogoro na nchi nzima kwa kuzingatia weledi wa kazi, nidhamu na uwajibikaji.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na Mkaguzi Mkuu wa Nje Mkoa wa Morogoro Bw. Mwabulanga A. Peter katika kikao cha baraza la madiwani cha kufunga kilichohudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Mbunge wa jimbo la Mikumi, madiwani na watendaji wa halmashauri ya wilaya ya Kilosa katika ukumbi wa Kilosa club.

Mkaguzi mkuu wa nje amesema kuwa Mkaguzi Mkuu wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaipongeza wilaya ya Kilosa kwa kumudu kuwa hati safi kwa miaka mitatu mfululizo huku akibainisha kuwa Kilosa ni miongoni mwa wilaya zilizoshika nafasi ya juu kati ya wilaya 138 nchi nzima zilizopata hati safi.

Aidha Bw. Mwaburanga ametoa rai kwa wilaya zote zilizopo katika Mkoa wa Morogoro kuiga mfano wa utendaji kazi wa Halmashauri wa Kilosa ambayo kwa miaka mitatu mfululizo ikishikilia rekodi ya kuwa na hati safi, ambapo amesema kuwa kwa ukaguzi wa mwaka 2016/2017 amezitaka wilaya za Mji Ifakara na Malinyi ambazo ni Halmashauri mpya kujifunza kwa Halmashauri ya wilaya ya Kilosa ili kupata hati safi.

Sambamba na hayo amewapongeza madiwani wa Halmashauri ya Kilosa kwa kusimamia vema Halmashauri kwani toka mwaka 2011 hadi 2016 Kilosa imekuwa ikipata hati inayoridhisha ikiashiria kuwa ni ishara njema ya nidhamu na uwajibikaji katika utendaji kazi kiujumla katika wilaya hii.



Mkaguzi Mkuu wa Nje mkoa wa Morogoro Bw. Mwaburanga A. Peter akisoma matokeo ripoti ya ukaguzi kwa Halmashauri ya wilaya Kilosa, ambapo katika matokeo hayo Kilosa imepata hati safi na kuwa miongoni mwa Halmashauri 138 nchini zilizofanya vizuri kwa mwaka wa fedha 2015/2016.